# TANGAZO

## TAARIFA YA UFAFANUZI KUHUSU MPANGO MAALUM WA KUWAREJESHA WATANZANIA WALIOKWAMA NCHINI INDIA

Ubalozi unapenda kufafanua kuhusu mpango maalum wa kuwarejesha watanzania waliokwama nchini India kama ifuatavyo:

1. Ubalozi unathibitisha taarifa iliyosambazwa kupitia **Kundi-Sogozi [Whatsup Group]** linaloratibiwa na **Bwana Andrew Demello** mwenye namba **+255784360859** kuwa ni taarifa sahihi na kwamba utaratibu alioueleza ndio unapaswa kufuatwa.

2. Ubalozi utahusika katika kuomba vibali vya "Air Tanzania" kutua katika Jiji la Mumbai tarehe 11 Mei 2020 kwa ajili ya safari ya tarehe 12 Mei 2020 ya Mumbai-Dar es Salaam. Aidha, Ubalozi utahusika katika kuwaombea vibali wale wote watakaokuwa wamelipia tiketi ya ndege hiyo ili waweze kutoka sehemu walipo na kufika Mumbai kwa ajili ya safari hiyo.

3. Ubalozi unasisitiza kuwa watanzania waliokuwa wamekwama nchini India baada ya kukamilisha matibabu na wanafunzi waliohitimu masomo yao kuchangamkia fursa hii adhimu.

4. Ndege itayotumika kwa safari hiyo maalum ni ndege ya Shirika la Ndege la "**AIR TANZANIA**"

**UBALOZI WA TANZANIA, NEW DELHI, INDIA**
**07 MEI 2020**